# UMOJA - JARIDA

UNITED NATIONS TANZANIA

Toleo la 89
Machi - Aprili 2020


## KUDUMISHA HAKI KATIKA KIPINDI CHA KUKABILIANA NA COVID-19



Haki za wanawake na wasichana hazina budi kupewa kipaumbele katika mapambano ya taifa dhidi ya COVID-19 nchini Tanzania. **Picha | *UNFPA Tanzania***

## VIDOKEZO


- UN Tanzania yalipa gharama za kufunga umeme kwa wakulima wa mwani Zanzibar
- FAO, SUA na Chuo Kikuu cha Jimbo la Kansas vyatoa mafunzo kwa wataalamu wa mstari wa mbele juu ya namna ya kupambana na COVID-19, Ebola
- Kutumia mafunzo ya Ebola ili kuzuia virusi vya corona kuingia katika kambi za wakimbizi nchini Tanzania
- Kizazi cha Usawa kwa Maendeleo ya Tanzania ya Sasa na ya Baadae


Angelina amefanya kazi ya ukunga kwa miaka 30. Hivi sasa anafanya kazi katika Hospitali ya Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu. Hivi karibuni, hospitali hii ilikarabatiwa na kuwekewa vifaa vipya na UNFPA ili itoe huduma bora za matunzo ya afya kwa mama na mtoto ikiwemo dharura za uzazi pingamizi na pia matunzo kwa watoto wachanga.

Angelina anasema hata baada ya kufanya kazi kwa miongo mitatu bado anajisikia fahari na furaha pale amwonapo mama anayetabasamu huku kwa mara ya kwanza akiwa amembeba mtoto wake mwenye afya njema... Hujisikia kutua mzigo. Mama yake Angelina alipoteza maisha wakati kujifungua.

Huku mgonjwa wa kwanza wa ugonjwa utokanao na virusi vipya vya Corona (COVID-19) akithibitishwa nchini Tanzania katikati ya mwezi Machi, Angelina ana mashaka makubwa. Bado hakuna wagonjwa walioripotiwa katika Wilaya ya Bariadi, lakini anasema kwamba jamii 'iko macho' na hofu yake kubwa ni namna atakavyoendelea kuwalinda akina mama na watoto wachanga endapo kutatokea idadi kubwa ya wagonjwa wa COVID-19 na huku yeye akiwa zamu.

Neema, ambaye ni mfanyakazi mwenzake Angelina katika Hospitali ya Wilaya ya Bariadi, amefanya kazi ya ukunga kwa miaka saba sasa,

*Inaendelea Ukurasa wa pili (2)*

*Kutoka ukurasa wa Kwanza (1)*

na hata yeye ana hofu na ugonjwa huu. "Ninapotazama taarifa za habari, najiuliza nini kitatokea endapo watu hawataruhusiwa kutoka majumbani mwao? Je, tutawafikisha vipi akina mama wajawazito katika vituo vya afya ili wapate huduma za kabla ya kujifungua, wakati wa kujifungua na baada ya kujifungua?" Pamoja na ustahimilivu na ujasiri walio nao Angelina na Neema, wa kuendelea kutoa huduma za kuokoa maisha kwa wajawazito na watoto wachanga, wanawake hawa wawili wana hofu pia kuhusu usalama wao binafsi.

UNFPA inashirikiana na Wizara ya Afya ili kuchukua hatua za kuhakikisha kwamba huduma bora na salama za afya ya mama, afya ya ngono na uzazi (SRH) zinapewa kipaumbele kama sehemu ya mwitikio dhidi ya COVID-19. Mahitaji ya taifa ya vifaa vya ya uzazi, zikiwemo njia za kisasa za kuzuia mimba na dawa za kuokoa maisha ya akina mama, vimetabiriwa kwamba huenda vikawa haba, na vifaa vya kitabibu vya kijikinga (PPE) na dawa muhimu za kuzuia maambukizi tayari zimenunuliwa kwa ajili ya vituo vya afya vya ngazi za mikoa, wilaya na ngazi za chini kwa mikoa ya Simiyu, Kigoma na Dodoma na Dar es Salaam na Zanzibar kwa visiwa vyote viwili vya Unguja na Pemba; vilevile, mafunzo na rasilimali yameandaliwa kwa ajili ya vituo hivyo katika mikoa hiyo.

Manesi wakunga na maofisa afya wanaendelea kuajiriwa tayari kukabiliana na ongezeko la mahitaji ya matunzo ya afya. Na kwa kutambua kwamba kipindi hiki kina shinikizo kubwa sana kwa wafanyakazi wa afya walio mstari wa mbele, wakiwemo manesi wakunga kama Angelina na Neema, UNFPA inafanya mpango kuandaa utoaji huduma za nasaha kwa wafanyakazi hawa kupitia njia za mtandao na kupitia kituo cha taifa cha msaada kwa njia za simu za bure na pia kupitia huduma za utumaji wa ujumbe ili kupata msaada kwa pande zote mbili za Tanzania Bara na Zanzibar.

UNFPA itaendelea kuweka kipaumbele katika kutoa kinga kwa wafanyakazi katika sekta ya Afya nchini Tanzania, na kuhakikisha kwamba haki za wanawake na wasichana, hasa wale walio hatarini zaidi, zinalindwa na kuweka uzito katika mwitikio wa kitaifa dhidi ya COVID-19 na kwamba wito wa kutomwacha yeyote nyuma hivi sasa unapaswa kupewa nguvu zaidi.

## UN TANZANIA YALIPA GHARAMA ZA KUFUNGA UMEME KWA WAKULIMA WA MWANI ZANZIBAR

Kama sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Umoja wa Mataifa mnamo tarehe 26 Oktoba, 2019, Mfumo wa Umoja wa Mataifa nchini Tanzania ulikisadia kikundi cha kuchakata mwani kinachoitwa Ukweli Ndio Njia cha Bweleo, Zanzibar kwa kukipa kiasi cha Shilingi za Tanzania milioni 2 ili kugharimia uwekaji umeme wa njia tatu katika kituo chao. Lengo la msaada huu ni kuimarisha uwezo wa uzalishaji katika uchakataji wa mwani huko Bweleo, na kwa hiyo kukuza mnyororo wa thamani wa bidhaa zitokanazo na mwani.

Kutokana na msaada huu, kiwanda hivi sasa kinazalisha sabuni zaidi kutoka miche 100 hadi 300 kwa siku. Ongezeko kama hilo linatarajiwa katika bidhaa nyingine ambazo zinachakatwa hapa. Kwa taarifa, tasnia ya kilimo cha mwani ni chanzo kikuuu cha mapato kwa Zanzibar baada ya utalii na kilimo cha karafuu na kinaajiri zaidi ya watu 24,000, ambapo miongoni mwao asilimia 80 ni wanawake.

Programu ya Pamoja ya Zanzibar (ZJP) ilizinduliwa na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar,

*Inaendelea Ukurasa wa tatu (3)*



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org | Website: www.tanzania.un.org | Tel: (+255) 22-219-5021

*Kutoka ukurasa wa pili (2)*

Mh. Dkt. Ali Mohamed Shein, mwaka 2018. Moja ya maeneo manne yaliyo chini ya Programu hiyo ni Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi Kupitia Ukuzaji wa Mnyororo wa Thamani katika Kilimo cha Mwani.






Tarehe 25 Machi 2020. Kushoto ni jengo la kiwanda ambalo taa zake zimewashwa usiku. Kulia ni mfumo wa kuzima umeme wa njia tatu. Umeme huo umefungwa kwenye jengo hilo ili kusaidia kikundi cha Ukweli Ndio Njia Safi kuongeza uzalishaji. **Picha | *UN Tanzania***

## FAO, SUA NA CHUO KIKUU CHA JIMBO LA KANSAS VYATOA MAFUNZO KWA WATAALAMU WA MSTARI WA MBELE JUU YA NAMNA YA KUPAMBANA NA COVID-19, EBOLA

Jumla ya wataalamu 55 wa mstari wa mbele kutoka katika wilaya zilizo hatarini zaidi wamapewa mafunzo ya namna ya kuzuia COVID-19, kugundua kwa haraka na uchukuaji sampuli kwa kutumia njia ya mfumo wa Kutoa Huduma za Haraka chini ya mpango wa *One Health* (OH).

Mafunzo hayo yaliendeshwa mwezi Machi mkoani Dodoma na yaliratibiwa na Dawati la Uratibu la One Health lililo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na kuwezeshwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO) kupitia mradi unaofadhiliwa na USAID wa Ajenda ya Usalama wa Afya Duniani (*Global Health Security Agenda* - GHSA). Mafunzo haya yaliendeshwa kwa ushirikiano na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE) kupitia Mradi wake wa *Veterinary Education Establishment Twinning* unaoendeshwa na Chuo Kikuu cha Jimbo la Kansas (KSU) na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA).

Kiongozi wa Timu ya Nchi ya FAO inayosimamia Programu ya Kituo cha Dharura cha Magonjwa ya Wanyama Yanayohama (*Emergency Centre for Transboundary Animal Disease* (ECTAD)), Bw. Fasina Folorunso, alisema mafunzo hayo yatasaidia kuimarisha mbinu za uratibu katika sekta-mseto katika ngazi za serikali za mitaa, kuimarisha uwezo wa kuendeleza One Health na kuwezesha njia za uratibu wa kuzuia, kutambua, na kutoa mwitikio kwa magonjwa ya kipaumbele yanayoruka kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu (PZDs) yakiwemo COVID-19 na Ebola.

"Katika siku za karibuni, mifumo ya afya duniani kote imepata changamoto kutokana na kuibuka na kujitokeza

*Inaendelea Ukurasa wa nne (4)*

*Kutoka ukurasa wa tatu (3)*

upya kwa magonjwa yanayoambukiza kama vile Ebola kule Afrika Magharibi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, janga lililopo la COVID-19 na magonjwa mengine mengi yanayohama kutoka kwa wanyama kuja kwa binadamu.

"Hapa nchini Tanzania tulilenga kuwawezesha wataalamu wa afya ya binadamu na wanyama katika maeneo yaliyochaguliwa maalumu kutokana na kuwa kwenye hatari zaidi ya Kagera, Kigoma, Katavi, Rukwa, Songwe na Dodoma katika kukabiliana na magonjwa haya," alisema.

Kwa mujibu wake, kuleta ufanisi katika kuzuia, kugundua na kutoa mwitikio kwa magonjwa yanayohama kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu ya kipaumbele kunahitaji njia ya uratibu wa sekta mseto na utoaji mwitikio na kwa hiyo ni muhimu kutumia njia ya One Health.

"Hii ni kwa kutambua kazi iliyofanywa na wadau mbalimbali katika kushughulikia kinga, utambuzi, uchukuaji hatua, utayari na mwitikio katika matukio na dharura za afya ya umma," aliongeza Fasina.

Uwekaji mipango na utekelezaji wa majukumu ulitambua uzoefu na rasilimali zilizopo katika Wizara ya Afya na ile ya Mifugo, Shirika la Afya Duniani (WHO), FAO, SUA na Chuo Kikuu cha Jimbo la Kansas na pia vita vinavyoendelea sasa dhidi ya janga la COVID-19.



Prof. Rudovick Kazwala wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) akiwaeleza washirika wa mafunzo jinsi ya kuvaa mavazi maalumu ya kujikinga *(Personal Protective Equipment (PPE)*. **Picha | *Fasina Folorunso.***

## KUTUMIA MAFUNZO YA EBOLA ILI KUZUIA VIRUSI VYA CORONA KUINGIA KATIKA KAMBI ZA WAKIMBIZI NCHINI TANZANIA

Wakati mlipuko wa Ebola ulipoikumba Afrika ya Magharibi miaka mitano iliyopita, Miata Tubee Johnson, mkimbizi wa zamani kutoka Liberia ambaye sasa ni ofisa wa afya ya umma wa UNHCR, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi, alifanya kazi kubwa muhimu ya kupunguza vifo katika jamii kutokana na ugonjwa huo hatari wa virusi ambao uliua zaidi ya watu 10,000.

Sasa kutokana na kuenea kwa COVID-19, anatumia maarifa yake ya kupambana

*Inaendelea Ukurasa wa tano (5)*



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org | Website: www.tanzania.un.org | Tel: (+255) 22-219-5021

*Kutoka ukurasa wa nne (4)*

na virusi ili kuwalinda maelfu ya wakimbizi walio kwenye hatari kubwa wanaoishi katika kambi nchini Tanzania. “Tunachotaka kuzuia kwa kila jinsi ni kutokea kwa mlipuko kambini,” anasema Miata, ambaye hutumia siku yake kati ya ofisi yake na kambi tatu za wakimbizi zilizoko mkoani Kigoma, Tanzania.

Zaidi ya robo tatu ya wakimbizi milioni 25.9 kote duniani wanaishi katika nchi zinazoendelea. Ili kuzuia vifo na mateso yanayoepukika, UNHCR inatoa kipaumbele katika hatua za kuchukua ili kuzuia mlipuko wa COVID-19 kwani endapo utatokea utaongeza mzigo mkubwa katika mfumo wa utoaji huduma za afya ambao tayari una matatizo mengi. “Tunachotaka kuzuia kwa kila jinsi ni kutokea kwa mlipuko kambini,” anasema Miata.

Wakati ambapo kuna takribani wakimbizi 245,000 nchini Tanzania, Miata anapambana kufa na kupona ili kuzuia kutokea kwa mlipuko katika makambi ya wakimbizi na katika jamii za wenyeji zilizo jirani. Jambo la kwanza katika ajenda yake ni kuongoza mikutano ya matayarisho ya COVID-19 na watumishi 20 kutoka katika mashirika tofauti na serikali, huku wakiwa wamekaa umbali wa walau mita moja kutoka kila mmoja chini ya mti – kufanya mazoezi ya kukaa mbalimbali.

Kisha, atakabidhi mashine za



Miata akikagua dawa na bidhaa dawa katika Kambi ya Mtendeli. **Picha | *UNHCR Tanzania/ Deogratius Dyurumushi***

X-ray za kidigitali ambazo zinahitajika sana na zilizonunuliwa kwa fedha za wahisani katika hospitali ya wilaya iliyo jirani inayotoa huduma kwa jamii za wenyeji. Mashine hizo ni vifaa muhimu katika utambuzi wa COVID-19, kwani husaidia kujua kiwango cha uharibifu katika mapafu. “Daima tunashughulika kujenga uwezo wa vituo vya afya vilivyo jirani pale tunapobaini upungufu fulani. Jambo hili ni muhimu ili kuwezesha jamii hizi mbili za wenyeji na wakimbizi kuishi pamoja,” anaongeza Miata.

Hadi sasa bado hakujawa na wagonjwa walioripotiwa nchini Tanzania kutokana na ugonjwa wa virusi vya corona miongoni mwa wakimbizi, wengi wao wakiwa kutoka Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Upande mmoja wa juhudi za Miata ni kuhakikisha wakimbizi wanajumuishwa katika shughuli za upimaji, utayari na mwitikio za kitaifa. “Endapo kutakuwa na wagonjwa wa COVID-19 kambini, hawa watahamishiwa katika hospitali zilizoteuliwa za serikali,” anaeleza.

Wakati ambapo chanzo cha COVID-19 na kuenea kwake ni tofauti na Ebola, Miata anatumia sana uzoefu wake wa kupambana na Ebola nchini Liberia ili kutoa ujumbe wa afya ya umma wenye lengo la kuokoa maisha na kutoa wito kwa kuunganishwa kwa mwitikio dhidi ya virusi vya corona wa wakimbizi na ule wa kitaifa. “Kwa kweli, uzoefu wangu nchini Liberia umeniandaa kukabiliana na yanayotokea leo.”

*Inaendelea Ukurasa wa sita (6)*

*Kutoka ukurasa wa tano (5)*

Huduma kwa wakimbizi nchini Tanzania ni miongoni mwa huduma zinazopokea fedha kidogo zaidi katika ukanda huu, ambapo imepokea asilimia 25 tu ya fedha zilizoombwa kwa 2019-2020. Matokeo yake ni kuwa huduma za msingi zinabeba mzigo mkubwa na hazikidhi kabisa mahitaji ya wakimbizi.




Miata akitoa maelezo kwa washirika kuhusu programu ya afya na uchukuaji hatua za kitabibu katika Kambi ya Wakimbizi ya Nyarugusu. **Picha | *UNHCR Tanzania/ Maimuna Mtengela***

## RIPOTI MAALUMU (I): KIZAZI CHA USAWA KWA MAENDELEO YA TANZANIA YA SASA NA YA BAADAE

***Picha | UN Tanzania/Grace Mongi & UN Women/Tsitsi Matope.**

Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake ya mwaka huu yalizinduliwa mnamo tarehe 27 Februari na Spika wa zamani wa Bunge, Mh. Anne Makinda, jijini Dodoma. Ujumbe wa kimataifa wa maadhimisho hayo ulikuwa: "Niko katika Kizazi chenye Usawa: Kuleta Haki za Wanawake". Ujumbe wa kitaifa ulikuwa: "Kizazi cha Usawa kwa Maendeleo ya Tanzania ya Sasa na ya Baadae". Uzinduzi ulihudhuriwa na zaidi ya watu 2,000 wakiwemo wajasiriamali ambao walionyesha bidhaa zao mbalimbali katika kituo cha maonyesho. Uzinduzi uliofanyika Dodoma ulikuwa sehemu ya mfululizo wa matukio ambayo hatimaye yalifikia kilele mkoani Simiyu mnamo Machi 8.

Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanawake, Bi. Hodan Addou, alikuwa miongoni mwa watoa mada ambapo aliuwakilisha Umoja wa Mataifa Tanzania. Alisema kwamba Kumbukumbu za Miaka 25 ya Tamko la Beijing na Jukwaa la Kuchukua Hatua zilitoa fursa kwa wadau wote kupima maendeleo yaliyopatikana katika kutekeleza kanuni ya ushirikiano katika madaraka na wajibu kati ya wanawake na wanaume majumbani, pahali pa kazi na katika jamii pana kitaifa na kimataifa.

Rais wa kwanza wa Bunge la Afrika, Dkt. Getrude Mongella, na mkuu wa mkoa wa kwanza

*Inaendelea Ukurasa wa saba (7)*



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org | Website: www.tanzania.un.org | Tel: (+255) 22-219-5021

*Kutoka ukurasa wa sita (6)*

mwanamke Tanzania, Mh. Anna Margareth Abdalla, waliwaasa wanawake na wanaume kuwapigia kura wanawake wengi zaidi kuingia Bungeni katika uchaguzi wa mwaka huu. Mh. Makinda alieleza kutoridhishwa kwake na hatua iliyopigwa hadi sasa katika usawa wa jinsia, miaka 25 baada ya kutiwa saini kwa Tamko la Beijing na Jukwa la Kuchukua Hatua. Alisema kwamba wanawake ambao wanafanya asilimia 51 ya idadi ya watu Tanzania wanapaswa walau kuwa na asilimia 20 ya wabunge wa kuchaguliwa Bungeni.

Dkt. Mongella alilitumia jukwaa kutangaza uzinduzi wa Mtandao wa Viongozi Wanawake wa Afrika, ambao alisema utawaleta pamoja viongozi wanawake bila kujali itikadi zao za kisiasa, hali zao za kijamii wala kiuchumi. Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mh. Ummy Mwalimu, alisema serikali inatekeleza mfululizo wa marekebisho ya sera, miongozo na kanuni ili kuimarisha haki za wanawake na watoto.

Mkoani Simiyu, zaidi ya watu 5,000 waliungana na maofisa wa ngazi za juu wa serikali na taasisi binafsi, wanawake wafanya biashara kutoka mkoani humo na mikoa mingine, wanafunzi na jamii za wenyeji katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake.



Mratibu Mkazi wa UN Tanzania, Bw. Zlatan Milisic, akirudia ahadi ya Umoja wa Mataifa ya kufikia viwango vya juu vya usawa wa jinsia na uwezeshaji wanawake na wasichana nchini Tanzania hapo ifikapo mwaka 2030 kama inavyohimizwa katika Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan alikuwa ndiye mgeni rasmi katika kilele cha maadhimisho, mkoani Simiyu. Alisisitiza umuhimu wa kuendelea kutoa kipaumbele, viwango vya juu zaidi vya elimu kwa wanawake na wasichana ili kupunguza tofauti za jinsia katika sekta mbalimbali zikiwemo siasa, utawala na mahakama. Kwa Tanzania Bara, alisema ni wanawake 126 tu ndiyo Wabunge (36.7%) wakati ambapo katika mahakama, kati ya majaji 72 wa Mahakama ya Rufani, wanawake ni 27 tu.

Kwa upande wake, Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa, Bw. Zlatan Milisic, aliangazia umuhimu wa kuongeza kasi ya kutekeleza Lengo la 5 la SDG la Usawa wa Jinsia ili kufikia malengo ya dunia ifikapo 2030. “Ifikapo 2030, hatuna budi kuishi katika dunia ambamo wanawake na wasichana wanapata elimu, matunzo ya afya na kazi zenye hadhi. Ifikapo 2030, tunapaswa kuishi katika dunia ambamo wanawake na wasichana wako huru dhidi ya ukatili na wanapata uwakilishi sawa katika michakato ya kufanya maamuzi ya kisiasa na kiuchumi,” alisema Bw. Milisic.

Mwakilishi wa UN Women, Bi. Addou alisema licha ya mafanikio makubwa katika kuelekea kwenye usawa wa jinsia nchini Tanzania, bado kuna kazi kubwa ya kufanya ili kufanya wanawake wapate haki zao.

Ili kufikia lengo hilo, alisema kuna haja ya kufanya kazi zaidi ili kuhakikisha kwamba ile hali ya umaskini kuwa na sura ya mwanamke inafutwa kabisa na kwamba wanawake wanapata usawa wa kweli katika kumiliki ardhi na mali,

*Inaendelea Ukurasa wa nane (8)*

*Kutoka ukurasa wa saba (7)*

kupata kazi zenye hadhi, na kuhamasisha mgawanyo sawa katika kazi zile zisizolipiwa.

Mratibu Mkazi wa UN Tanzania, Bw. Milisic, alirejea ahadi ya Umoja wa Mataifa ya kuleta usawa wa jinsia na kuwawezesha wanawake na wasichana nchini Tanzania hapo ifikapo mwaka 2030 kama inavyoaswa kupitia Malengo ya Maendelea Endelevu (SDGs).



Makamu wa Rais, Mh. Samia Suluhu Hassan, akipewa maelezo kuhusu baadhi ya kazi ambazo UNFPA inafanya mkoani Simiyu wakati alipotembelea Banda la Umoja wa Mataifa katika Maonyesho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake mkoani humo. Kulia kwake ni maofisa wa UNFPA na katikati kulia ni Mwakilishi wa UNFPA nchini Bi. Jacqueline Mahon.



Balozi wa Kanada nchini Tanzania, Mh. Pamela O'Donnel, akitoa hotuba yake kwa niaba ya washirika wa maendeleo nchini Tanzania. Alijenga hoja kuhusu umuhimu wa kuongeza ushirikiano katika juhudi za Serikali za kufikia usawa wa jinsia na uwezeshaji wanawake na wasichana nchini Tanzania.

*Inaendelea Ukurasa wa tisa (9)*



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org | Website: www.tanzania.un.org | Tel: (+255) 22-219-5021

*Kutoka ukurasa wa nane (8)*



(Kutoka kushoto kwenda kulia) Balozi wa Canada nchini Tanzania, Mh. Pamela O'Donnel; Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mh. Ummy Mwalimu; Makamu wa Rais, Mh. Samia Suluhu Hassan; Mratibu wa Umoja wa Mataifa Tanzania, Bw. Zlatan Milisic; na Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Mh. Anthony Mtaka, wakipokea maandamano wakati wa maadhimisho ya mafanikio ya wanawake na wasichana nchini Tanzania katika sherehe za Siku ya Kimataifa ya Wanawake.




Taasisi mbalimbali zikiwemo za Serikali, UN, AZAKI na washirika wa maendeleo wakiandamana kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Wanawake. Maandamano hayo yalilenga kuonyesha kuwa wanawake wanaweza kufanya kazi mbalimbali ambazo kwa muda mrefu zimekuwa zikifanywa na wanaume tu ikiwemo kuendesha malori.

*Inaendelea Ukurasa wa kumi (10)*

*Kutoka ukurasa wa tisa (9)*



Faustina Mfinanga, ambaye ni maarufu kama Nandy 'The African Princess', mwanamuziki wa mitindo ya 'Bongo Flava' akitumbuiza kwa wimbo maalumu kuhusu uwezeshaji wanawake wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake.




Mamia ya wakazi wa mkoa wa Simiyu wakishiriki katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake.



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org | Website: www.tanzania.un.org | Tel: (+255) 22-219-5021

# RIPOTI MAALUMU (II): MAADHIMISHO YA SIKU YA KIMATAIFA YA WANAWAKE HUKO ZANZIBAR




Bi. Julia Broussard, Naibu Mwakilishi wa UN Women nchini Tanzania, akitoa salamu wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake huko Zanzibar. Alizungumza kwa niaba ya Mfumo wa Umoja wa Mataifa nchini Tanzania. **Picha | *UN Women***

'Mimi ni mwanamke bora kabisa; mimi ni mwanamke bora kabisa'. Hii ilikuwa ni kauli mbiu katika asubuhi nzuri ya Jumapili katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake katika ukumbi wa Idriss Abdul Wakil huko Zanzibar. Mgeni rasmi alikuwa ni Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Bi. Mgeni Hassan.

Maadhimisho hayo yalikwenda sambamba na kampeni ya dunia ya Kizazi cha Usawa na kuendelezwa katika ujumbe wa Zanzibar wa "Endeleza vuguvugu la kuleta usawa: Zingatia Haki za Wan¬awake". Ili kufikia lengo hili, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto iliandaa kongamano lililojikita katika kutathmini utekelezaji wa Tamko la Beijing na Jukwaa la Kuchukua Hatua kwa upande wa Zanzibar. Kongamano lilikazia maeneo manne: Wanawake na Elimu; Wanawake na Afya; Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi; na Kumaliza Ukatili dhidi ya Wanawake na Wasichana.

Akizungumza kwa niaba ya Umoja wa Mataifa Tanzania, Naibu Mwakilishi kutoka UN Women, Bi. Julie Brous¬sard, alisema:"Umoja wa Mataifa unathibitisha ahadi yake ya kuwa mshirika wa kuaminika katika kuhamasisha usawa wa jinsia na kutokomeza aina zote za ubaguzi na ukatili dhidi ya wanawake na wasichana."

Bi. Sabra Machano, Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Zanzibar (ZSSF), aliwasihi wanawake kutokukaa katika uhusiano uliojaa mateso kisa watoto, bali aliwataka kusimama imara dhidi ya uonevu kwa lengo la kujilinda na kuwalinda watoto wao.

Baadhi ya mapendekezo yanayotokana na kongamano hilo ni pamoja na: 1) Kuwashajiisha manusura wa vitendo vya ukatili wa kijinsia kutumia Vituo vya Kutolea Taarifa ili kupata huduma za afya na za aina nyinginezo; 2) Kusisitiza mwendelezo wa juhudi za kuwawezesha wanawake kujua haki zao ba binadamu; na, 3) pendekezo la kuwa na mahakama maalumu ambayo inaweza kufanyia kazi kwa kwa haraka na kutolea uamuzi wa haraka masuala ya vitendo vya ukatili kwa msingi wa jinsia. Kwa kuongezea, kulikuwa na wito wa kufanya takwimu zinazowahusu wanawake na wasichana Zanzibar zipatikane na zitumike.

Kongamano lilifungwa na Bi. Mgeni Hassan, ambaye pia alikuwa mwenyekiti wake na kutumia fursa hiyo kuwashajiisha wanawake kugombea na kushiriki katika uchaguzi unaokuja.

*Inaendelea Ukurasa wa kumi na mbili (12)*

*Kutoka ukurasa wa kumi na moja (11)*




Washiriki wakipiga picha na mgeni rasmi, Mh. Mgeni Hassan, ambaye ni Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar (mstari wa mbele, katikati). **Picha | *UN Women***




Bi. Sabra Machano, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) akiwahimiza wanawake kusimama kidete dhidi ya ukatili wa kijinsia. **Picha | *UN Women***



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org | Website: www.tanzania.un.org | Tel: (+255) 22-219-5021

# MAOFISA WA UN WAUNGANA NA SERIKALI NA WATU WA ZANZIBAR KATIKA MWITIKIO DHIDI YA COVID-19

Mapema mwezi Aprili, maofisa wa Umoja wa Mataifa katika Ofisi ya Zanzibar walitoa mchango mdogo kwa Wizara ya Afya ya Zanzibar ili kukidhi baadhi ya mahitaji muhimu katika kituo cha kuhudumia na kutoa tiba kwa wagonjwa wa COVID-19 cha Kidimni, Unguja. Katika taarifa fupi kutoka Umoja wa Mataifa, Bw. Ali Shaib, Msaidizi wa Masuala ya Fedha wa UNDP, alieleza kwamba maofisa hao wa UN waliguswa na juhudi za kitaifa katika mwitikio dhidi ya maambukizi ya COVID-19 huko Zanzibar, na mchango huo ulikuwa ishara ya ahadi zao binafsi katika kuendelea kupambana na COVID-19 huko Zanzibar.

Mchango huo ulipokewa na Mwenyekiti wa Kikosi Kazi cha Taifa cha Wizara ya Afya cha COVID-19, Dkt. Jamala Taib, ambaye alitoa shukrani kwa niaba ya Wizara. Mchango huo ulilenga mahitaji ya haraka kwa wafanyakazi na wagonjwa katika kituo hicho cha Kidimni, zikiwemo sabuni, viimo vya kunawia mikono, pedi za hedhi salama na viti.

Umoja wa Mataifa umekuwa ukiisaidia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika uratibu wake wa mwitikio dhidi ya COVID-19 katika sekta mbalimbali, zikiwemo kikosi kazi cha taifa cha sekta ya afya dhidi ya COVID-19. Kwa kuongezea, Umoja wa Mataifa umekuwa ukitoa misaada ya dharura ya kiufundi na mahitaji, yakiwemo vifaa maalumu vya madaktari kujikinga (*personal pro¬tection equipment* (PPE)), Usafirishaji Salama wa Sampuli za Virusi (*Viral Transport Medium* (VTM)), vifungashio vya ngazi tatu, mafunzo na uanzishwaji wa Timu za Mwitikio wa Haraka za Wilaya na Taifa (RRTs), mafunzo kuhusu namna ya kuhudumia wagonjwa wa COVID-19 kwa usalama, ukusanyaji wa sampuli za maabara ikiwemo kuzuia na kudhibiti maambukizi na utekelezaji wa utoaji taarifa za hatari na namna ya kuishirikisha jamii.



Maofisa wa Umoja wa Mataifa wakikabidhi misaada mbalimbali kwa Dkt. Jamala Taib, Mkurugenzi Mkuu katika Wizara ya Afya. Misaada hiyo inalenga kusaidia juhudi za kupambana na COVID-19 katika Kituo cha Kuhudumia na Kutibu Wagonjwa wa COVID-19 huko Zanzibar. **Picha | *UN Tanzania***

# ILO YATOA MAFUNZO YA KUNOA UJUZI VIJANA NA MAOFISA WA SERIKALI KUPITIA KJP




Washiriki wakishirikishana jambo wakati wa kipindi cha mafunzo kwa wakufunzi kuhusu Anzisha na Imarisha Bishara Yako (SIYB). **Picha | *ILO/Cressida Mwamboma***

Mnamo mwezi Machi, Shirika la Kazi Duniani (ILO), kupitia mradi wa Uwezeshaji Vijana na Wanawake Kiuchumi wa Mpango wa Pamoja wa Kigoma (KJP), liliendesha mafunzo ya kunoa ujuzi kwa kulenga vijana Watoa Huduma za Kuanzisha Biashara, maofisa wa serikali za mitaa na wawakilishi kutoka katika Ofisi ya Sekretariati ya Mkoa wa Kigoma ili kuhakikisha kwamba vijana hao wanaendelea kutoa huduma kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa kupitia mafunzo ya wajasiriamali vijana na wanawake wakati na hata baada ya Mpango wa KJP kukamilika.

Mafunzo hayo yalikazia kuimarisha uwezo wa vijana watoa huduma hizo, kwa kushirikiana na serikali za mitaa, kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana na wanawake wajasiriamali na hivyo kuwezesha uanzishaji wa biashara imara na kudumisha uendelevu wa biashara zinazoendeshwa na vijana na wanawake kupitia programu ya ILO ya Anzisha na Imarisha Biashara Yako (Start and Improve Your Busi¬ness (SIYB)). Ili kufikia lengo hili, mada mbalimbali za biashara zikiwemo kununua na kutunza vizuri mali iliyopo, ukaguzi wa gharama, utafutaji masoko, waajiriwa na ufanisi wao, uwekaji mipango na vilevile utunzaji wa kumbukumbu vinavyoainishwa katika zana za ILO za Imarisha Biashara Yako (Improve your Business (IYB)) zilifundishwa.

Vilevile, kupitia warsha hii, washiriki walipitia utekelezaji wa mipango kazi iliyoandaliwa na kupitishwa wakati wa mafunzo ya mwanzo ya wakufunzi yaliyofanyika mwezi Agosti, 2019. Sehemu ya mapitio hayo ilihusisha utoaji wa dodoso fupi kwa wakufunzi. Kupitia majibu yao, tangu mafunzo ya mwanzo ya mwezi Agosti, 2019, wakufunzi wameweza kuwafikia vijana na wanawake wajasiriamali zaidi ya 1,000 ambao walifaulu kuandaa mipango kazi kwa ajili ya biashara za vikundi na kuimarisha utendaji wa biashara zao. Kufuatia maendeleo haya, baadhi ya vikundi vinavyosimamiwa na wakufunzi vimefaulu kupata mikopo inayotolewa na serikali za mitaa inayolenga vijana na wanawake. Wakufunzi wanakiri kwamba kumekuwa na uimarikaji katika uendeshaji biashara na usimamizi wa vikundi umekuwa mwepesi zaidi.

Katika mipango ya baadaye, progamu inakusudia kuendelea kusimamia watoa huduma waliopata mafunzo na maofisa wa serikali za mitaa ikiwemo kuwawezesha kama wakufunzi waliothibishwa.

*Inaendelea Ukurasa wa kumi na tano (15)*



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org | Website: www.tanzania.un.org | Tel: (+255) 22-219-5021

*Kutoka ukurasa wa kumi na nne (14)*



Bw. Lawrence Ambokile, mkufunzi kuhusu mpango wa ILO wa Start and Improve Your Business (SIYB), akiendesha kipindi kwa wakufunzi wa SIYB mkoani Kigoma kama njia ya kuimarisha uwezo wa Watoa Huduma za Uanzishaji Biashara na maofisa wa serikali za mitaa ili waweze kutoa elimu kwa vijana na wanawake wajasirimali kuhusu ujasiriamali mkoani Kigoma. **Picha | *ILO/Cressida Mwamboma***



Bi. Godliver Mtaheba, mmoja wa washiriki wa mafunzo ya Anzisha na Imarisha Biashara Yako akieleza jambo kuhusu namna ya kuimarisha mafunzo kwa wanufaika katika wilaya zilizo kwenye programu hiyo. **Photo| *ILO/Cressida Mwamboma***

# UNICEF YATOA MSAADA WA VIFAA VYA KIJIKINGA NA KUWASAIDIA WATU KIJIKINGA DHIDI YA COVID-19



Wanawake wa Dar es Salaam wakisoma bango lenye ujumbe kuhusu COVID-19 katika kituo cha basi. Hili ni moja ya mabango yanayosambazwa na Chama cha Msalaba Mwekundu kupitia msaada wa UNICEF. **Picha | *UNICEF Tanzania***

Wakati ambapo Tanzania inapambana na janga la COVID-19, UNICEF inaisaidia Serikali ya Tanzania katika vita hivyo kwa kuipatia misaada muhimu ya kiufundi ili kuokoa maisha na kuwashirikisha wajenga ushawishi katika jamii wakiwemo viongozi wa dini, vyombo vya habari na wale wa mitandaoni kuwa wahamasishi wa mabadiliko ya tabia ili kuzuia kuenea kwa virusi.

Ili kuhakikisha usalama wa watumishi wa afya, UNICEF imeagiza mavazi maalumu ya kujikinga (PPE) na bidhaa nyingine za dharura zenye thamani ya Dola za Marekani US$ 550,000. Vifaa hivyo vinatarajiwa kuwasili nchini kabla ya mwisho wa mwezi Mei. Zaidi ya hayo, PPE zilizotengenezwa hapa nchini zenye thamani ya Dola za Marekani US$ 910,000 zitapatikana ifikapo mwanzo wa Juni.

Kama mwenyekiti mwenza wa Kikosi Kazi cha Usimamizi wa Mawasiliano wakati wa Hatari na Ushirikishwaji wa Jamii (RCCE) pamoja na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, UNICEF imesaidia kuwaleta pamoja zaidi ya washirika 70 ili kujiunga katika harakati hizi (taasisi za hapa nchini na za kimataifa, vikundi vya kitaalamu, mashirika rafiki na mashirika ya Umoja wa Mataifa) kwa Tanzania Bara na Zanzibar.

Kupitia Kikosi Kazi cha RCCE, UNICEF imeisaidia Serikali kuanzisha kampeni za nchi nzima kupitia vyombo vya habari zikiwa na ujumbe unaolenga kuzuia kuenea, ikiwa ni pamoja na kuwalinda wale walio hatarini zaidi. Takribani maudhui tofauti 120 yamewafikia zaidi ya watu milioni 15 wakiwa nyumbani mwao kupitia redio za kitaifa na zile za jamii, runinga na vyombo vingine vya habari.

*Inaendelea Ukurasa wa kumi na saba (17)*



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org | Website: www.tanzania.un.org | Tel: (+255) 22-219-5021

*Kutoka ukurasa wa kumi na sita (16)*

Majukwaa ya mitandao ya kijamii na ushirikishwaji wa wasanii na wajenga ushawishi wa mitandaoni unaendelea kuwafikia watu wengine wapatao milioni 3-4 kila wiki.

Ili kupima ueneaji wa ujumbe na mabadiliko ya maarifa, mitazamo na tabia, UNICEF imeanzisha utafiti unaoendelea katika mikoa 8 kwa Tanzania Bara na Zanzibar. Wakati huohuo, kura za maoni kupitia ujumbe mfupi wa simu (U-Report SMS) na ujumbe wa WhatsApp unasaidia kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji upotoshaji ili kuona maeneo ya kufanyia marekebisho katika juhudi zinazoendelea.

Washirika kama vile Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania wanaisaidia UNICEF kusaidia juhudi katika ngazi ya jamii katika miji mikubwa ambako watu 10,471,594 (59%) katika jumla ya watu 17,682,684 wamefikiwa, wakati ambapo pikipiki na spika kubwa zimetumika kufikia maeneo yasiyofikika kwa urahisi hasa wakati wa msimu wa mvua.

UNICEF inasaidia katika juhudi za ufuatiliaji katika jamii kwenye mikoa iliyo hatarini zaidi upande wa Tanzania Bara kupitia utoaji mafunzo kwa Maofisa Afya wa Jamii na ambao wataanza kupelekwa kwenye vituo vya kazi kuanzia katikati ya Mei. Na kupitia msaada wa UNICEF, wakimbizi 192,288 katika Kambi tatu za Nyarugusu, Nduta na Mten¬deli wanawezeshwa kunawa mikono baada ya kuwekewa ndoo za maji na sabuni za maji. Kazi kubwa ya Timu ya C4D katika maeneo yote kwenye Muundo wa RCCE imehakikisha kuwa masuala muhimu kama vile kinga ya watoto, VAC, vitendo vya ukatili kwa msingi wa kijinsia yanashughulikiwa, wakati ambapo ujuzi na rasilimali kama vile Maji na Usafi wa Mazingira vinatumika, na mahitaji ya makundi yaliyo katika hali ngumu zaidi yanazingatiwa kadiri ya mwitikio wa RCCE.

Matumizi ya ushawishi wa viongozi wa dini ni njia moja muhimu katika kuhamasisha ujumbe wa kuzuia kuenea kwa COVID-19, kutoa miongozo kuhusu uendeshaji ibada ulio salama na kufanya maziko yenye kuonyesha heshima kwa waliofariki, ambapo kampeni zenye kutafakarisha zilizoshirikia viongozi wa imani za Kikristo na Kiislamu zilisaidia kuhamasisha ibada kutokea majumbani, unawaji mikono na ukaaji wa mbalimbali. Vipindi viwili kupitia webinar na viongozi wa Kiislamu na Kikristo nchini Tanzania, Afrika na India vilisaidia kujenga uongozi imara katika kuweka ahadi imara za kuanzisha na utetezi miongoni mwa waumini wao na jamii kwa ujumla.

## MATUKIO YAJAYO YA SIKU ZA KIMATAIFA

**Mei 22 –** Siku ya Kimataifa ya Uanuai wa Kibiolojia
**Mei 23-** Siku ya Kimataifa ya Kukomesha Fistula na Uzazi Pingamizi
**Mei 29 –** Siku ya Kimataifa ya Walinda Amani wa Umoja wa Mataifa
**Juni 5 –** Siku ya Mazingira Duniani
**Juni 7 –** Siku ya Usalama wa Chakula Duniani
**Juni 8 –** Siku ya Bahari Duniani
**Juni 13 –** Siku ya Kimataifa ya Kutoa Elimu Juu ya Ualbino
**Juni 20 –** Siku ya Wakimbizi Duniani

UNITED NATIONS
TANZANIA

UMOJA WA MATAIFA IMARA KWA DUNIA ILIYO BORA ZAIDI

**Umoja wa Mataifa Tanzania**
+255 22 219 5021
info.untz@one.un.org
Website: tanzania.un.org